

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA HANDENI

Simu ya mdomo:	027 - 29 77402
Tel Fax:	027- 29 77402
E-mail:	ded@handenidc.go.tz
Kumb. yako :	
Kumbu yetu :	HW/S.20/96/5



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (H/W)
S.L.P. 355,
Handeni, Tanga,
Tanzania

21/03/2018

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni anawatangazia Watanzania wenye sifa kujaza nafasi wazi za Watendaji wa Vijiji kwa kibali cha ajira mbadala kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora chenye Kumb. Na. CFC. 26/205/01 "GG"/95 cha tarehe 12 Machi, 2018 kuajiri nafasi Thelathini na Tano (35).

MTENDAJI WA KIJIKI III (Nafasi 35)

A. Sifa, Elimu na Ujuzi

Mwombaji awe na elimu ya kidato cha nne au cha sita na kuhitimu Astashahada/cheti katika fani Utawala, Sheria, Fedha, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Jamii kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali.

B. Ngazi ya Mshahara

Cheo cha Mtendaji wa Kijiji III kina ngazi ya mshahara TGS B

C. Kazi/Majukumu ya Mtendaji wa Kijiji III

- i/ Kukusanya mapato ya Halmashauri ya Wilaya.
- ii/ Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji;
- iii/ Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji;
- vii/ Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji;
- v/ Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji;
- vi/ Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu;
- vii/ Kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa Kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali;
- viii/ Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika Kijiji;

- ix/ Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na Nyaraka za Kijiji;
- x/ Mwenyekiti wa Kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji;
- xi/ Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

MASHARTI YA JUMLA KWA NAFASI ZOTE

- i/ Mwombaji awe Mtanzania mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- ii/ Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono na kutumwa kwenye anwani iliyotajwa hapo chini.
- iii/ Mwombaji aambatanishe nakala za vyeti vya kiadato cha nne/sita, vyeti vya taaluma, cheti cha kuzaliwa. maelezo binafsi (CV) na nyaraka zote muhimu pamoja na picha 2 (passport size) zilizopigwa hivi karibuni. Aidha TESTIMONIALS, PROVISIONAL RESULTS, STATEMENT OF RESULTS HAVITAKUBALIWA.
- iv/ Kwa wale waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (NECTA na TCU) na taarifa ya uhakiki iambatanishwe kwenye maombi.
- v/ Kwa wale watakaopita kwenye mchujo wa awali (Short listed candidates) ndio watakaoitwa kufika kwenye usaili (Interview) na kufika na vyeti halisi.
- vi/ Nafasi ya kazi aliyoomba iandikwe juu ya bahasha, kutozingatia hili kutasababisha maombi ya kazi kuwa batili.
- vii/ Barua zote za maombi zitumwe kwa anwani ifuatayo;

**MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA HANDENI,
S. L. P 355,
HANDENI.**

Aidha, uwasilishaji wa barua za maombi kwa mkono katika Ofisi za Halmashauri ya Wilaya hautakubalika na barua hizo hazitapokelewa..

Mwisho wa kutuma na kupokea maombi ni tarehe 03 Aprili, 2018 Saa 9:30 alasiri.


.....
William M. Makufwe
**Mkurugenzi Mtendaji (H/W)
HANDENI.**

**MKURUGENZI MTENDAJI (H/W)
HANDENI**

Nakala: Mbao zote za matangazo.
Halmashauri ya Wilaya
HANDENI.